**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 01 Oktoba, 2024**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

143. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Kwa kiasi gani viongozi wa dini wanatoa mchango wao katika jamii na kupambana na vitendo vya rushwa.

(b) Kwa namna gani Serikali inawawezesha katika mapambano hayo.

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Kuna aina ngapi za ngazi za madaraja ya udereva katika utumishi wa umma.

(b) Tathmini iko vipi juu ya viwango vya mishahara ya madereva hao kulingana na madaraja yao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

262. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2021 ni nyenzo muhimu katika kusimamia masuala yote ya ununuzi hapa Zanzibar. Pamoja na kwamba Sheria hii tayari imepitwa na wakati, bado ina mambo mengi ambayo kwa kiasi kikubwa inafanya utekelezaji wa masuala ya ununuzi kuchelewa na kuwa na gharama kubwa.

(a) Kwa kuzingatia muda wote tokea kutungwa kwake hadi leo, Je, haijatosha kwa Serikali kuitambua kuwa Sheria hii imepitwa na wakati na kuna haja ya kuifanyia mabadiliko.

(b) Je, Serikali ina ufahamu wowote kwamba Kanuni za Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma za mwaka 2021, kwa kiasi kikubwa haziiakisi Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

265. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hivi karibuni, Serikali imeanzisha mpango wa kutoza Dola 44 ($.44) kama bima ya lazima kwa wageni wote wanaoingia Zanzibar, ambapo mpango huu utaanza kutumika tarehe 01 Oktoba 2024. Hata hivyo, hatua hii imeibua malalamiko kutoka kwa wadau na wataalamu wa utalii wa Zanzibar.

(a) Je, Serikali imefanya tafiti na kujiridhisha kwamba mpango wa kutoza bima hii hautaathiri Sekta ya Utalii Zanzibar.

(b) Je, ni sababu zipi zilizofanya mpango huu kutochukuliwa katika bajeti ya Wizara husika kabla ya kutangazwa kwa umma.

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuja na mpango huu ni kwenda kinyume na miongozo ya Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC) juu ya uhuru wa mtalii kukata bima katika nchi anayotaka na katika chombo anachotaka.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

125. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

(a) Serikali inasimamia vipi suala zima la uajiri na haki za waajiriwa katika sekta binafsi hususani kupitia kada za ualimu na mahoteli ya kitalii.

(b) Kwa vipi na kwa namna gani Serikali imeweza kutatua changamoto za wafanyakazi wa mahoteli na waajiri wao.

(c) Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa inayoonesha ni kwa asilimia ngapi changamoto hiyo imepungua.

126. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kumekuwa na baadhi ya malalamiko kutoka kwa wafanyakazi wa baadhi ya mahoteli kwa waajiri wao kuwanyanyasa, kuwabeza, kuwapa vitisho, kuwafukuza kiholela na hata kuwatolea lugha za kibaguzi.

(a) Je, tathmini ya Wizara yako iko vipi juu ya tatizo hili kwa sasa.

(b) Kwa kiasi gani Wizara yako inafuatilia kwa karibu sana na kuyapatia ufumbuzi malalamiko haya pindi yanapojitokeza.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

134. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tumeshuhudia mwaka huu kuwa siku ya Kiswahili Duniani iliadhimishwa kwa hamasa kubwa kupitia mataifa mbali mbali Duniani, mnamo tarehe 07/07/2024.

Ni kwa namna gani Zanzibar kama chimbuko la Kiswahili sanifu tuliweza kuiadhimisha siku hii adhimu na ya kipekee.

148. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kila taifa linajivunia watu wake mashuhuri walioyaletea mataifa yao heshima na umaarufu mkubwa usioweza kusahaulika.

Je, ni watu gani mashuhuri sana katika tasnia ya michezo, ubunifu na sanaa hapa Zanzibar, ambao Serikali haitaweza kusahau michango yao daima.

**Wizara ya Afya:**

115. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la wagonjwa wa maradhi ya kukosa usingizi.

(b) Mpaka hivi sasa tuna madaktari bingwa wangapi waliobobea kwenye tatizo hili.

116. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tatizo la kupoteza kumbukumbu kwa watu wazima limekuwa likiongezeka zaidi kuliko hali ilivyokuwa kwa miaka ya nyuma.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea tatizo hili kuongezeka kwa kasi kubwa.

(b) Nini tiba mbadala ya tatizo hili.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

211. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

(a) Kwa kiasi gani Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imeweza kufanikiwa kupunguza migogoro ya wananchi katika muktadha huo.

(b) Ni lini posho na stahiki za Wajumbe wa Bodi hiyo zilizolimbikizwa kwa kipindi kirefu, zitapatiwa ufumbuzi ili kuleta ufanisi katika utendaji wa Bodi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

83. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizowahi kutembelewa na wageni mbali mbali mashuhuri duniani akiwemo Queen Victoria na Dr. David Living Stone.

Je, ni maeneo au vitu gani ambavyo vinahifadhiwa mpaka sasa vinavyoashiria ujio wa ugeni huu mashuhuri katika kuienzi historia ya Zanzibar na kuikuza zaidi sekta ya utalii.

84. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Je, kuna ukweli wowote juu ya uwepo wa njia za chini kwa chini zinazozunguka eneo la kihistoria la Mji Mkongwe.

(b) Kuna utafiti wowote uliofanyika au kutaka kufanyika ambao unahalalisha ukweli huu au utaweza kutoa majibu yanayotarajiwa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

103. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

(a) Ni aina gani ya zao la mwani ambayo Wizara yako inawashajiisha wakulima wa mwani kuipanda kwa lengo la kujikimu vizuri kimaisha.

(b) Tathmini iko vipi juu ya ubora wa mwani unaozalishwa nchini katika uhitaji wa soko la kimataifa.

(c) Maeneo gani ni vinara wa kuzalisha mwani kwa wingi na kwa kiwango kinachokubalika.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

34. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa kiholela hasa za vyakula.

Je, ni wakati gani Serikali hulazimika kuingilia kupanda kwa bei za bidhaa hapa Zanzibar.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2023/2024.

.

**Zanzibar,**
**01 Oktoba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARA**